# KCPE 2008

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1–50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**21.** Udogo wa neno **mtoto** ni:
   A. jitoto
   B. kitoto
   C. toto
   D. mtoto

Jibu sahihi ni B

**Katika karatasi ya majibu:**

1 [A] [B] [C] [D]   11 [A] [B] [C] [D]   21 [A] [▬] [C] [D]   31 [A] [B] [C] [D]   41 [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **21**, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

**Maswali 1 mpaka 15.**

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Kwa __1__ Kiswahili ni lugha ya Kiafrika ambayo imeenea kote. Wenyeji asilia __2__ wakiongea lugha hii __3__ awali ni Waswahili. Waswahili wanapatikana kote katika upwa mzima __4__ pwani ya Afrika Mashariki. Kwa muda mrefu Kiswahili __5__ humu nchini lakini mambo yamebadilika. Lugha hii sasa imepewa hadhi kubwa __6__ nyanja mbalimbali nchini. Lugha hii __7__ pakubwa kuwaunganisha wananchi na kudumisha amani. Wakenya wengi wamejitolea kuikuza lugha hii yao na hawataki tena __8__.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | sababu | hivyo | hakika | vile |
| **2.** | wamekuwa | waliokuwa | watakaokuwa | wangekuwa |
| **3.** | tangu | hadi | hata | mpaka |
| **4.** | wa | kwa | ya | mwa |
| **5.** | hakikudhaminiwa | haikuthaminiwa | haikudhaminiwa | hakikuthaminiwa |
| **6.** | katika | kati ya | ndani ya | kuliko |
| **7.** | imechanga | imechangiwa | imechangia | imechangisha |
| **8.** | kuizungumza | kuitwaza | kuitumia | kuididimiza |

Arusi ya Hadija __9__ kijijini mote. Nyimbo zilisikika kwa siku tatu mfululizo. Vigoli na maghulamu walicheza ngoma bila kusita. __10__ ya magari ilionekana __11__ kuelekea msikitini kwa sherehe ya kufunga ndoa. Kijiji chote kilijaa wageni __12__ kutayarisha arusi. Nyumba ya bibiarusi ilijaa mapambo tele na kuta __13__ kupakwa rangi ya kupendeza. Arusi ikawa ya kufana mno. Watu __14__. Hata baada ya __15__ nilienda nikijisemea kimoyomoyo, "Jambo la heri huenda kwa heri. Mola awajalie mema."

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| **9.** | ilitia chumvi | ilitia fora | ilipiga mbiu | ilipiga debe |
| **10.** | Safu | Milolongo | Msongamano | Msitari |
| **11.** | ikiandamana | ikifuatia | ikifuatwa | ikiandama |
| **12.** | walivyokuja | walipokuja | waliyokuja | waliokuja |
| **13.** | yoyote | yote | zote | zozote |
| **14.** | wameiajabia | wanaiajabia | wakaiajabia | wakiiajabia |
| **15.** | kutangamana | kujumuika | kufungamana | kufumukana |

*Kutoka swali la* **16** *mpaka* **30**, *chagua jibu lililo sahihi.*

**16.** Chagua usemi wa taarifa ulio sahihi wa
"Kilele cha Mlima Kenya kina theluji nyingi."
Fatuma akasema.
A. Fatuma alisema kwamba kilele cha Mlima Kenya kilikuwa na theluji nyingi.
B. Fatuma anasema kwamba kilele cha Mlima Kenya huwa na theluji nyingi.
C. Fatuma akasema kwamba kilele cha Mlima Kenya kimekuwa na theluji nyingi.
D. Fatuma alisema kwamba kilele cha Mlima Kenya kingekuwa na theluji nyingi.

**17.** Ni sentensi ipi inayoonyesha matumizi sahihi ya **Lau**?
A. Lau mwanafunzi anapopita mtihani hutuzwa.
B. Lau ungekuja ningekusaidia.
C. Nipe lau kitabu kimoja nisome.
D. Nitakujuza lau hutaki kujua.

**18.** Chagua jibu linaloonyesha aina za mashairi.
A. Tarbia, Takhmisa
B. Tarbia, Mizani
C. Vina, Takhmisa
D. Takhmisa, Mishororo

**19.** Chagua kinyume cha sentensi:
Musa alisifiwa kwa utiifu wake.
A. Musa hakusifiwa kwa utiifu wake.
B. Musa alikashifiwa kwa utundu wake.
C. Musa alikashifiwa kwa ukaidi wake.
D. Musa hakukashifiwa kwa ukaidi wake.

**20.** Methali yenye maana sawa na "usiache mbachao kwa msala upitao" ni
A. usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi
B. bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi
C. usipoziba ufa utajenga ukuta
D. bura yangu siibadili na rehani.

**21.** Jogoo ni kwa koo, fahali ni kwa
A. ndama
B. kipora
C. tembe
D. mtamba

**22.** Chagua aina ya pambo ambalo huvaliwa miguuni.
A Kipete
B. Kidani
C Kikuku
D. Kikuba

**23.** Umoja wa sentensi "Waungwana wowote hawawezi kutufanyia fujo" ni
A. Muungwana yeyote hawezi kutufanyia fujo.
B. Muungwana yeyote hawezi kunifanyia fujo.
C. Muungwana yoyote hawezi kunifanyia fujo.
D. Muungwana yoyote hawezi kutufanyia fujo.

**24.** Chagua sentensi ambayo ni muungano sahihi wa hizi:
Mburukenge aliingia uwanjani.
Mburukenge aliwafadhaisha wanafunzi.
A. Mburukenge aliingia uwanjani na kuwafadhaisha wanafunzi.
B. Mburukenge aliingia uwanjani kwa kuwafadhaisha wanafunzi.
C. Mburukenge aliingia uwanjani lakini aliwafadhaisha wanafunzi.
D. Mburukenge aliingia uwanjani kwani aliwafadhaisha wanafunzi.

**25.** Kumpiga mtu vijembe ni
A. kumpa sifa asizostahili
B. kumsema kwa mafumbo
C. kumchafulia mtu jina
D. kumfanyia ishara ya dharau.

**26.** Ugonjwa wa **ukambi** pia huitwa
A. surua
B. safura
C. ndui
D. tetewanga

**27.** Sahihisha: Kule mlikolima hamna rutuba.
A. Kule mlipolima hamna rutuba.
B. Pale mlipolima hamna rutuba.
C. Kule mlikolima hakuna rutuba.
D. Mle mlimolima hakuna rutuba.

**28.** Chagua nomino kutokana na kitenzi **kumbuka**:
A. Kumbukika
B. Kumbukwa
C. Kumbusha
D. Kumbusho.

**29.** Umbu, mkoi, halati,wote ni
A. jamii
B. wakwe
C. jamaa
D. marafiki.

**30.** Kitendawili "Nikitembea yuko, nikikimbia yuko, nikiingia ndani hayuko," jibu lake ni
A. mwanga
B. kivuli
C. mwangwi
D. upepo

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 – 40.*

Uamuzi uliofanywa na serikali wa kuhimiza watoto wote warudi shuleni ni jambo mwafaka. Watoto walifurika furifuri shuleni ili kusajiliwa. Wale waliokuwa wakirandaranda mitaani walifuatilizwa himahima na kupelekwa shule. Waliokuwa wakubwa ki-umri walipelekwa kwenye shule za ufundi. Wakatabasamu kwa furaha kama mzazi aliyepata salama.

Kwa miaka mingi, baadhi ya wazazi walikuwa wameshindwa kuwasomesha wana wao. Hii ni kutokana na umaskini uliokithiri mipaka. Hali hiyo ilichangia huzuni kuu miongoni mwa familia. Pengo la waliosoma na wasiosoma lilizidi kuwa pana kielimu na kiuchumi. Uadui ukaingilia jamii. Ujambazi nao ukazidi.

Sasa watu wote wakipewa haki sawa ya kusoma, hata wale watoto wa maskini watamanio masomo watakinaisha kiu yao. Pia mengi ya matatizo yatapungua. Si kweli kuwa tajiri ni mwerevu kuliko mkata. Kila mwanajamii akipewa nafasi na asome kwa bidii atafua dafu maishani.

Vijana watakaofuzu katika shule za kiufundi wataweza kuajiriwa katika sekta mbalimbali. Mwishowe wakipata mtaji watajiendeleza kwa kuanzisha miradi midogomidogo ya kujitegemea. Hali kama hii ikienea kote nchini viwanda vidogovidogo vitaanzishwa na ajira itapatikana. Hiyo itakuwa njia mojawapo kuu ya kuinua uchumi na kuzalisha nafasi nyingi za kazi. Kitaaluma, hawa vijana wataweza kuwa madaktari, wasanii, walimu ... na kazi zingine nyingi. Kisomo ni kitamu. Hakifai kutiliwa nanga.

31. Uamuzi uliofanywa na serikali
   A. ulisababisha kufurika kwa watoto shuleni na kupita mitihani.
   B. ulisababisha kuchipuka kwa vyuo vya ufundi na kuondoa umaskini.
   C. ulisababisha kuongezeka kwa watoto shuleni na kupata nafasi ya kujiendeleza.
   D. ulisababisha kupungua kwa umaskini na kuwapa watoto nafasi ya kujiendeleza.

32. ...baadhi ya wazazi walikuwa wameshindwa kuwasomesha wana wao.
   Chagua methali inayoweza kuelezea hali hii.
   A. Maskini kupata ni mwenye nguvu kupenda.
   B. Dau la mnyonge haliendi joshi.
   C. Ngombe wa maskini hazai pacha.
   D. Maskini halali mchana.

33. Ukosefu wa elimu unasababisha
   A. umaskini, uadui, huzuni na ujambazi
   B. wivu, ujambazi, kukosa kiu ya kusoma na uadui
   C. utajiri, ukosefu wa kazi, huzuni na ujambazi
   D. ujambazi, wivu, utajiri na kiu ya kusoma.

34. Kulingana na kifungu, pengo kubwa la kiuchumi limesababishwa na
   A. watoto kutopata kisomo kwa sababu ya umaskini
   B. uadui na ujambazi uliokumba jamii maskini
   C. watoto kutopelekwa shule za ufundi kwa sababu ya umaskini
   D. wazazi kushindwa kupambana na umaskini.

35. Ni kweli kuwa watu wote wakipewa nafasi sawa
   A. watoto wa maskini watakuwa werevu
   B. watoto maskini na tajiri watakuwa sawa
   C. watoto wote wapendao kusoma watakuwa matajiri
   D. watoto wote wapendao kusoma watapata kisomo.

36. Vijana wote wakipata mtaji:
   A. wataanzisha miradi ya kiufundi
   B. wataweza hata kuwa wataalamu
   C. wataanzisha shughuli za kujikimu
   D. watakitilia kisomo chao makini.

37. Kisomo hakifai kutiliwa nanga kwa sababu
   A. watu watakuwa wataalamu
   B. kina manufaa mengi
   C. shule zitapanuka
   D. serikali itakigharamia.

38. Maana ya kusajiliwa ni:
   A. kurekebishwa
   B. kunufaishwa
   C. kuandikishwa
   D. kufundishwa.

39. Watakinaisha kiu yao kwa maana ya:
   A. watapunguza tamaa yao
   B. wataacha hofu yao.
   C. watafurahia hali yao.
   D. watatosheleza hamu yao.

40. Kichwa kinachofaa zaidi kwa taarifa hii ni:
   A. Ukarimu wa serikali.
   B. Kupunguza ujinga.
   C. Masomo ya kiufundi.
   D. Serikali kupanua masomo.

*Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.*

Wanafunzi wa shule ya Mtepetevu walitembelewa na wazazi. Kabla ya kuruhusiwa kukutana na watoto wao, wazazi waliingia kwenye mkutano. Takriban kila mzazi alimbebea mwanawe furushi la chakula, licha ya kuwa watoto wao walikuwa wamerudi kutoka nyumbani majuma mawili tu yaliyopita.

Mkutanoni wazazi walizozana kuhusu maakuli shuleni, mavazi na mitindo ya nywele ya watoto hao. Baadhi walitaka watoto wao wapewe mapochopocho na matunda ghalighali. Wengine wao siku hiyo hawakufikiria sana kuhusu juhudi za watoto masomoni, kinyume na kawaida yao. Hata hivyo, wengi wao waliona mbele, wakapinga udekezaji huo.

Mzozo ulipokuwa ukipamba moto, kijana mmoja wa karibu miaka ishirini na minne, aliyekuwa amevalia kilalahoi, akaingia mkutanoni. Baadhi ya wazazi waliomuona walishindwa kwani mkutano ulikuwa ni wa wazazi. Kijana akaketi na kutega sikio. Mzazi mmoja alisimama na kusema, "Nimeitazama orodha hii ya vyakula na nimesikitika. Kwa nini hawa watoto hawapewi chapati kwa kima, pilau na 'matoke'? Tunalipa! Sasa kwa nini wanakula ugali na '*githeri*'".

Kijana yule alikereketwa, akaunyoosha mkono juu sana na alipoona anapuuzwa, akasimama na kuanza kusema, "Hoja mnazotoa si ...." Baadhi ya wazazi wakamdakia na kusema, "We! Nyamaza. U mtoto! U mkwe wetu...". Kijana akazidi kukakawana na kutaka kupewa nafasi lakini wale waliokuwa karibu naye wakamlazimisha kuketi. Mwenyekiti akasema, "Huu ni mkutano wa wazazi. Jukumu lako kijana ni kunyamaza na kusikiliza kwa makini, kisha uwapelekee wazazi ujumbe."

Kijana alikazana, "Tafadhali nipeni ruhusa. Kitanda msichokilalia, hamuwajui kunguni wake." Akaulizwa walikokuwa wazazi wake kwani ndio waliotakiwa mkutanoni. Akajibu, "Bwana Mwenyekiti, sina wazazi! Mimi ni mlezi wa wadogo zangu, nina mdogo wangu hapa. Nimetoka mbali huko kote kuja kuwawakilisha marehemu wazazi wangu. Mimi si mlevi, si mhuni au mkwe wenu. Nina akili razini. Kuwa kijana si dhambi. Nimemaliza chuo kikuu. Nina kazi lakini mshahara wote unaishia kwenye malezi na sasa mnanikataza kusema lolote. Je, kijana hana haki? Ninajua kuwa maji mengi hayazuiliki lakini tushirikianeni kwani penye wengi hapaharibiki neno".

Mwenyekiti akampa nafasi ya kujieleza. Kijana akaendelea, "Mimi kama kijana mlezi, nimewasikiliza kwa makini. Ninapinga hoja ya mavazi ya nyumbani na mapochopocho kama chapati....Jambo linalofaa ni kuwafunza kutafuta elimu kwa bidii. Wakihimizwa kuwa na adabu na kuwa na kiu ya masomo, watajikataza wenyewe kufuata tu raha maishani. Kula bila kujua kutafuta kutawatia mashimoni. Mvumilivu hula mbivu. Kugeuza mandhari ya shule kuwa ni sehemu ya mandari kutajenga uvivu, wizi, matabaka na wivu shuleni. Wanafunzi watawabeza walimu, badala ya kuwasikiliza. Tuwafunze kujitegemea". Wazazi walimhurumia na kumpigia makofi. Mwenyekiti akamuomba msamaha na kumshukuru kwa niaba ya wazazi.

**41.** Ni jambo gani linaloonyesha kuwa hawa watoto wanadekezwa?

A. Ingawa walikuwa hawajakaa sana shuleni, wazazi waliwabebea mafurushi ya vyakula.

B. Walikuwa wametoka nyumbani na mafurushi ya vyakula.

C. Wazazi walikuwa wanataka watoto wale mapochopocho, sio tu kuvaa kifahari.

D. Wazazi walikuja mpaka shuleni kuwaona watoto hao na vyakula.

**42.** Ukipamba moto maana yake ni:

A. ukiwa na joto jingi

B. ukizidi kuendelea

C. ukiharibika

D. ukihimizwa

**43.** Mkutanoni kulikuwa na:

A. wapinzani, mwenyekiti na kijana

B. waungaji mkono, kijana na mwenyekiti

C. wageni, kijana na mwenyekiti

D. wadekezaji, waona mbele na mwenyekiti

**44.** Kijana alipuuzwa kwa sababu ya

A. mavazi yake

B. mazungumzo yake

C. umri wake

D. kutaka kuongea.

**45.** Kwa nini kijana alikazana kunyoosha mkono?

A. Alitaka kuondoa shaka ya wazazi na kutoa hoja zake.

B. Alitaka kusema kuwa yeye ni mlezi si mkwe.

C. Alikasirika na kutaka kupingana na wazazi.

D. Alikasirika kwa kudharauliwa akataka ajitambulishe.

**46.** Hoja za kijana zilionyesha:

A. ukaidi wake

B. ulala hoi wake

C. ukomavu wake

D. ujana wake

**47.** Kulingana na kifungu kitanda msichokilalia hamuwajui kunguni wake ina maana

A. wazazi hawajajua matatizo ya watoto

B. wazazi hawakujua hali ya kijana

C. wazazi hawakuamini hoja za kijana

D. wazazi hawakuamini maoni ya watoto.

**48.** Kulingana na taarifa hii wazazi walipaswa

A. kujadili jinsi watoto wao walivyokula, walivyovaa na kuwa na mandari shuleni

B. kuzungumzia nidhamu na jinsi ya kuwahimiza walimu kuwapa watoto chakula cha kifahari

C. wakomeshe udekezaji, wahimize nidhamu na kuacha kutaka kugeuza shule kuwa ni mandari

D. kuondoa udekezaji na raha zote zilizokuwapo shuleni kama mavazi ya kifahari na lishe bora.

**49.** Mpangilio bora wa matukio ya siku hiyo huko Mtepetevu ulikuwa

A. kuwasili, kuingia mkutanoni, kuzozana, kuelewana na kuomba msamaha

B. kuwasili, kuzozana, kuomba msamaha, kuingia mkutanoni na kuelewana

C. kuwasili, kuingia mkutanoni, kuelewana, kuzozana na kuomba msamaha

D. kuwasili, kuzozana, kuingia mkutanoni, kuomba msamaha na kuelewana.

**50.** Kichwa mwafaka kinachofaa kuelezea taarifa hii ni:

A. Dhifa ya wazazi shuleni.

B. Ujana shuleni si hoja.

C. Mzozo na mapatano shuleni.

D. Kudunishwa kwa vijana shuleni.